

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



SALAM ZA MWAKA MPYA 2023

www.ludewadc.go.tz

Desemba 31, 2022

LUDEWA, NJOMBE

Mkuu wa wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere anawataka wananchi wote wa wilaya ya Ludewa na watanzania wote wanaoishi ndani ya Wilaya ya Ludewa kusheherekea sherehe ya Mwaka Mpya 2023 kwa Amani na Utulivu.

Katika maandalizi kuelekea Sikukuu ya Mwaka mpya 2023 Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mheshimiwa Tsere amewataka Wananchi Wilayani Ludewa kusherehekea Sikukuu hiyo kwa Amani na utulivu.

Mkuu wa Wilaya ametoa salamu hizo leo Desemba 31, 2022 Wilayani Ludewa, alipozungumza na Afisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Chrispin Kalinga kwa njia ya simu alipokuwa akipokea Taarifa ya maandalizi ya tamasha la 9 la wafanyabiasha linaloendelea Maisala Mjini Magharibi Zanzibar.

Mhe. Tsere amewashukuru wananchi kwa kudumisha amani na utulivu katika kipindi chote cha Mwaka 2022 ambapo amewataka Wananchi kuongeza juhudi zaidi na kuhakikisha kuwa Mwaka ujao 2023 Wilaya ya Ludewa inaendelea kwa kila sekta haswa katika mazao ya chakula pamaja na kufungua milango ya uwekezaji katika sekta ya Kilimo na maandalizi ya kuwahudumia wageni wanaokuja kuwekeza katika sekta ya Madini.

Amewataka wananchi kumaliza mwaka kwa kuhudhuria nyumba za ibada kila mmoja kwa Imani yake kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumaliza Mwaka 2022 salama.

“Ndugu yangu Kalinga naomba waambie wananchi wa Wilaya ya Ludewa kuwa, Mwaka ujao 2023 uwe ni Mwaka wa kufanya kazi kwa bidii zaidi ili kuhakikisha kuwa kila mmoja wetu anapata tija, Wilaya yetu inapata tija na Taifa letu linapata tija, katika maeneo yetu kila Kiongozi ahakikishe kazi zinafanyika kwa kiasi ili kupata tija ambayo Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameagiza tuongeze tija katika uzalishaji na Tija kwa Asilimia 10 ifikapo 2030.”

Sambamba na hayo Kama mnavyotambua Wilaya ya Ludewa ni Wilaya ya Kilimo hivyo nawasihi wananchi kuendelea na maandalizi kwani tayari mbolea imefika hivyo ni wajibu wetu kuipata mbolea hiyo kwa ajili ya mazao tuliyoalima. Amesema Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere.

Chrispin B. Kalinga

Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini

Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Makaa ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.